

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

Kumb. Na. HWI/S.10/16/60

25, MEI, 2022

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

### 1.0 UTANGULIZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ilaje baada ya kupokea kibali cha ajira chenye **Kumb Na. FA 97/228/01/9cha tarehe 13 Mei 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anawatangazia raia wa Tanzania wenyewe sifa kujaza nafasi wazi Nne (4) za Katibu Muhtasi**

### 2.0 KATIBU MUHTASI DARAJA LA III - (NAFASI 04)

#### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliohuduria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za **Windows, Microsoft office, Internet, E-mail na Publisher.**

#### 2.2 MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida ;
- (ii) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- (iii) Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.

- (iv) Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- (v) Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- (vi) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- (vii) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangwiwa na msimamizi wake wa kazi.

### **3.0 MAELEKEZO YA JUMLA**

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi 45.
- Waombaji waambatishe wasifu binafsi (Curriculum Vitae) anwani inayotumika,namba ya simu na anwani ya barua pepe (e-mail address) na majina ya Wadhamini(Referees) watatu.
- Waombaji waambatanishe cheti cha Kidato cha Nne, cheti cha kuzaliwa, Cheti cha kufuzu uhazili chenye hati mkato(Kiswahili na Kiingereza)
- Matokeo ya Muda (provisional/Testimonial/Statement Result)havitakubaliwa
- Waombaji watakaowasilisha vyeti vya kughushi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.
- Waombaji wenyе vyeti vya kidato cha Nne vya Nje ya Nchi vitatakiwa vithibitishwe na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
- Barua ya maombi itatakiwa iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza ikielekezwa kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Ileje kwa anuani tajwa hapo chini.
- Waombaji waambatanishe kitambulisho cha Uraia (National Identification Number) kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA),

kitambulisho cha Mpiga Kura na Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa kata/kijiji/Mtaa kutoka eneo unaloishi

- Kila barua ya muombaji iambatishwe na picha mbili ndogo (Passport Size) iliyopigwa siku za karibuni, anwani kamili ya makazi pamoja na namba ya simu.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta,barua zitakazowasilishwa mkononi hazitapokelewa wala kufanyiwa kazi.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na namba za simu za kuaminika Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09 Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri

#### 4.0 MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Ileje,  
S.L.P. 2,  
ILEJE

Geofrey M. Nhauye  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

*Geofrey M. Nhauye*  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
S. L. P. 2  
ILEJE  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya wilaya ya Ileje ambayo ni [www.ilejedc.go.tz](http://www.ilejedc.go.tz)